**SAS NOTES**

**KUZUNGUMZA NA WANAFUNZI WA DARASA LA VI NA VII WA SHULE YA MSINGI YA MWALIMU JULIUS KAMBARAGE NYERERE: UKUMBI WA MHASIBU HOUSE, DAR ES SALAAM ALHAMISI, 4 SEPTEMBA 2003**

# "UMOJA WA NCHI HURU ZA AFRIKA (OAU) KUUNDWA KWAKE MAFANIKIO NA MATATIZO NA SABABU ZA KUUNDWA NA MATARAJIO YA UMOJA WA AFRIKA (AU)"

## (1) UTANGULIZI

- Shukrani kwa Mwalimu Mkuu MWANTUMU MAHIZA kwa mwaliko.
- Umuhimu wa Vijana wetu na jamii yetu kwa jumla kuelewa OAU na AU – Tulipotoka na Tunapoelekea.

## (2) MADA

Nimeombwa nizungumzie Umoja wa Nchi Huru za Afrika; mambo yaliyosababisha kuundwa kwake; Mafanikio na Matatizo yake; sababu za kuundwa kwa Umoja wa Afrika (AU) na matarajio ya Umoja huo.

- Mada hii ni kubwa lakini nitajaribu nieleze kwa ufupi ili mupate nafasi ya kuuliza maswali.

## (3) MAMBO YALIYOSABABISHA KUUNDWA KWA OAU

(i) Historia fupi ya Afrika Baada ya Mkutano wa Berlin 1884 na taathira zake.

- Afrika ilivyogawika.

- Koloni za Waingereza – k.m. Nigeria, Ghana, Kenya, Uganda, Tanzania n.k.
- Koloni za Wafaransa – Côte d'Ivoire, Senegal, Algeria, Morocco, Benin, Chad n.k.
- Koloni za Wabelgiji – Congo (Kinshasa), Rwanda, Burundi.
- Koloni za Wareno – Msumbiji, Angola, Guinea Bissau, Sao Tome, Cape Verde.
- Koloni za Wahispania (Spain) – Equatorial Guinea, Sahara ya Magharibi.

(ii) Licha ya Mgawanyo huo pia kulikuwa na mgawanyiko wa:

(a) Kiitikadi – Nchi zilizoitikadiwa ni za kimapinduzi na zile za muhafidhina.

- Vikundi mbalimbali – Cassablanca *Group* (Morocco, Ghana, Guinea, Algeria, Mali na Algeria *Provisional Government.)*
- Monrovia *Group*
- Brazzaville *Group.*

(b) Kijiografia – Afrika, Kaskazini mwa Sahara na Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara.

(c) Kwa hiyo sababu moja kubwa ya kuanzishwa kwa OAU ni kuleta uelewano na mshikamano baina ya nchi za Kiafrika kwa lengo la kupigania haki za Waafrika.

- Pia hali halisi ya Kimataifa (VITA BARIDI) ilihitaji Umoja na Mshikamano wa nchi changa. Kwa mfano Umoja wa Nchi Zisizofungamana Upande Wowote ulianzishwa 1961 huko Belgrade, Yugoslavia.
- Muhimu kutambua kwamba pamoja na kuwepo na vikundi mbalimbali, hakuna nchi, kiongozi au kikundi

waliokuwa hawapendelei umoja kwa maslahi na mustakabali wa Mwafrika.

## (4) KUUNDWA KWA OAU

(i) Mwaliko wa *Emperor* Haile Selassie

- Viongozi wa Nchi Huru walikuwa Addis Ababa na kuanzisha OAU Mei 1963 (25 May - Africa Day)

(ii) Katiba (*Charter*) ya OAU ilikuwa na Malengo mengi. Ya msingi ni Mawili:

- Umoja wa watu wetu katika fani mbalimbali – Kisiasa, Kiuchumi, Kijamii na nyanja mbalimbali za Maendeleo.
- Kutumia nguvu za Umoja kuleta ukombozi wa Bara zima kutoka Ukoloni na Ubaguzi wa Rangi.

(iii) MIUNDO (*STRUCTURES*) ZA OAU

- Mkutano wa Viongozi (*Assembly*)
- Mkutano wa Mawaziri wa Nchi za Nje (*Council of Ministers*)
- *Secretariat* – Katibu Mkuu na Manaibu Katibu Mkuu watano (5)

N.B. OAU imekuwa na Makatibu Wakuu 6 – moja akiwa ni Katibu Mkuu wa muda naye ni Marehemu Peter Onu wa Nigeria. Maelezo kamili ni kama ifuatavyo:

1964 – 1972 – Bwana Diallo Telli (Guinea)

1972 – 1974 – Bwana Nzo Ekangaki (Cameroon)

1974 – 1978 – Bwana William Eteki Mboumoua (Cameroon)

1978 – 1983 – Bwana Edem Kodjo (Togo)

1983 – 1985 – Dr. Peter Onu (Nigeria)

1985 – 1989 – Bwana Ide Oumarou (Niger)

1989 – 2001 – Dr. Salim Ahmed Salim (Tanzania)

2001 – 2003 – Bwana Amara Essy ( Cote d'Ivoire)

## (5) MAFANIKIO YA OAU

(A) Kujenga na Kudumisha Umoja na Mshikamano (*African Identity*)

(B) Kuunga mkono vuguvugu la ukombozi Kisiasa, Kidiplomasia, Kinyenzo na Kijeshi

- Mchango muhimu wa Kamati ya Ukombozi – *OAU Liberation Committee* – iliyokuwa na Makao Makuu yake hapa Dar es Salaam
- Tanzania ilichangia kwa hali na mali. Wapigania Uhuru kupewa hifadhi na mafunzo; Silaha kupitishwa hapa.
- *Role* ya Makatibu Watendaji walioteuliwa na Tanzania – Marehemu Balozi Sebastian Charle na Balozi George Magombe na Baadaye Brigadier General (Mstaafu) na sasa Balozi wa Tanzania huko Zimbabwe, Hashim Mbitta.
- Mafanikio ni kamilifu:

Tokea nchi 32 (1963) hadi nchi 54 (ukiingiza Morocco)

(C) MAFANIKIO KATIKA USHIRIKIANO WA KIUCHUMI NA KIJAMII

1970 – 1990s – Mikakati mbalimbali ya kuleta ushirikiano wa karibu zaidi wa kiuchumi. Kwa mfano – Mpango wa Lagos 1980. Mkataba wa Abuja 1991 (kuhusu Jumuiya ya Kiuchumi ya Afrika). Kuanzishwa kwa Taasisi mbalimbali za kanda za Ushirikiano k.m. ECOWAS, ECCAS, COMESA, SADC, UMA, IGAD,

(D) Kuimarisha Utekelezaji wa Haki za Binadamu

- Mkataba wa Afrika kuhusu Haki na Wajibu wa Binadamu (*Africa Charter on Human and Peoples Rights*)
- *Commission*
- Makao Makuu yake Banjul, Gambia.

(E) KUTANZUA kwa kiwango fulani Migogoro

- Chombo maalum cha kutanzua migogoro (OAU *Mechanism in Conflict Prevention, Management and Resolution*)
- Chombo hiki kiliundwa 1993 huko Cairo kufuatia uamuzi wa Viongozi kujadili na kujaribu kutanzua matatizo ya ndani ya nchi za Afrika.

**(6) MATATIZO YA OAU**

- OAU ilishirikisha zaidi Dola na Waafrika wengi wa kawaida hawakuwa wanajua yanayotokea.
- Kuyumba-yumba kwa baadhi ya nchi kutokutekeleza maamuzi: Maamuzi mengi mazuri na ya kihistoria – utekelezaji mdogo.
- Kutokufaulu kuyapatia ufumbuzi wa kudumu migogoro ambayo taathira zake ni kubwa, kwa mfano Wakimbizi zaidi ya milioni 4 na IDPs zaidi ya milioni 10.
- UFINYU WA NYENZO.

**(7) KUUNDWA KWA AU** (Sababu zake na Muundo)

- Kuimarisha Umoja kulingana na mabadiliko ya hali ya Kimataifa.
- Kuyaendeleza mafanikio ya OAU na kuyaacha mbali yale yasiyokuwa na manufaa kwa wakati huu.
- Kutilia mkazo ukombozi wa kiuchumi kwa vile ukombozi dhidi ya ukoloni ulimalizika.

<u>Tarehe muhimu</u>

(a) Tamko la Sirte 9.9.99. Kutaka kuanzishwa kwa Umoja wa Afrika. (Mkutano uliofanyika huko Libya kwa mwaliko wa Kiongozi Muamar Al Gaddafi.)

(b) Kupitishwa kwa Katiba ya AU (*Constitutive Act*), Lome, 11 Julai 2000.

(c) Kikao cha dharura cha Viongozi wa OAU – Sirte, 2 Machi 2001 – waliohudhuria wote walikuwa wameshaweka saini.

(d) 25 Aprili 2001 – nchi 36 zilikwisha ridhia (2/3 *majority*)

(e) 26 Mei 2001 – Katiba ilianza kufanya kazi.

(f) Mkutano wa Lusaka (2001) ulikubaliana kipindi cha mpito cha mwaka mmoja. Mkutano wa Durban (2002) ambako AU ilitangazwa rasmi – kipindi cha mwaka mmoja zaidi kiliongezwa.

## (8) TAASISI MBALIMBALI ZA AU

17 kwa jumla – pamoja na *Assembly; Executive Council*, Kamati ya Wawakilishi wa Kiuchumi, *Commission*, Bunge, Taasisi za Fedha – (*African Central Bank, African Monetary Fund* na *African Investment Bank*).

## (9) MATARAJIO YA AU

- Chombo kiwe chachu ya ukombozi wa kiuchumi na maendeleo ya jamii ya watu wetu.
- Kuzingatia na kutanzua migogoro baina ya nchi na ndani ya nchi (kupitia *African Peace and Security Council*).
- Kuimarisha mshikamano na ushirikiano ili tuweze kukabili changamoto ya dunia ya utandawazi (*globalization*).
- Kulinda na kutetea haki za Mwafrika na Bara letu kwa jumla.

- Kuhakikisha kwamba Waafrika jumla yao wanashiriki katika harakati za Umoja huu.

## (10) CHANGAMOTO ILIYOPO MBELE

- Kufanikisha kuwa Taasisi zote zinafanya kazi. Hivi sasa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti na Wajumbe Saba (akiwemo Mtanzania Bibi Rose Kurijila) wameshachaguliwa kutoka Kikao cha huko Maputo, Julai 2003.
- Suala la *Sovereignty* na maslahi ya pamoja ya bara letu.
- Suala la Nyenzo na hasa fedha. Mfano kusaidia kutanzua migogoro kunahitaji fedha nyingi.

## (11) MWISHO

Kutoka OAU kwenda AU si badiliko la jina tu:

NJIA PEKEE YA BARA LETU KUWA NA SAUTI YA KUSIKILIZWA KATIKA MIDANI YA KIMATAIFA NI KUPITIA CHOMBO HICHI CHETU CHA AU.